

# JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM


**PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO**

S.L.P. 280 D'SALAAM, +255 686 794177, E: katolikimshikamano@gmail.com




## MATANGAZO: DOMINIKA YA 1 YA KWARESIMA A - TAREHE 22.02.2026

| | | |
|---|---|---|
| 1. | LEO DOMINIKA<br>22.02.2026<br>HARAMBEE MAALUM | **DOMINIKA YA 1 YA KWARESIMA MWAKA A**<br>Mchango wa pili ni kwa ajili ya Kuwezesha Mazishi ya Mpendwa Baba yetu Mwadhama Porlycard Kardinali Pengo |
| 2. | IJUMAA<br>20.02.2026 | Njia ya Msalaba saa 10:30 jioni ikiongozwa na WAWATA na itafuatiwa na Misa Takatifu. Kwa kipindi cha Kwaresma, siku za Ijumaa hakutakuwa na Misa za asubuhi.<br>Matoleo kipindi cha Kwaresma ni kwa ajili ya Kampeni ya Kwaresma |
| 3. | JUMAMOSI<br>28.02.2026 | Misa ya mazishi ya Mpendwa Baba yetu Mwadhama Porlycard Kardinali Pengo, Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam yatafanyika katika Kituo cha Hija Pugu. Misa itaanza saa 4:00 Asubuhi. Wote tunaalikwa kushiriki. |
| 4. | SEMINA, MAFUNGO NA HIJA YA VIONGOZI | Semina, Mafungo na Hija ya viongozi wa Halmashauri ya Walei Parokia katika Kituo cha Hija Boko ilifanyika jana Jumamosi 21.02.2026. Tunawapongeza na kuwashukuru viongozi 108 wa Kamati Tendaji za Jumuiya, Kamati Tendaji za Kanda na Kamati Tendaji za Vyama vya Kitume Parokia waliotenga muda wao na kushiriki. |
| 5. | DOMINIKA<br>01.03.2026 | **DOMINIKA YA 2 YA KWARESIMA MWAKA A**<br><br>**Misa ya 1: Saa 12:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Bernadetha<br>Watangaza Neno: Modesta Lyimo na Emmanuel Raphael<br>**Misa ya 2: Saa 2:30 asubuhu**<br>Wasimamizi: Bikira Maria Mpalizwa Mbinguni<br>Watangaza Neno: Agatha Kifaru na Fred Ngowi<br><br>**Misa ya 3: Saa 5:00 asubuhi**<br>Wasimamizi: **Mt Bernadetha na Bikira Maria Mpalizwa Mbinguni**<br>**Mchango wa pili kwa ajili ya ujenzi.** |
| 6. | VIWAWA | Jumamosi ijayo kutakuwa na mafungo ya Vijana wote hapa Parokiani yatakayoanza saa 3:00 asubuhi. Vijana wote wanaalikwa kushiriki.<br><br>**HIJA YA VIJANA JIMBO:** Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam Henry Mchamungu anawaalika Vijana wote kushiriki katika Hija ya Vijana Jimbo itakayofanyika 07.03.2026 katika kituo cha Hija Pugu |

| | | |
|---|---|---|
| | | kuanzia 02:00 - 10:00 jioni. **Mtukio:** Njia ya Msalaba, Semina, Maungamo na Misa Takatifu. Kila Jumuiya inaombwa kuchangia kiaasi cha 20,000 kwa ajili ya vijana wawili. |
| 7. | UWAKA | UWAWA wakutakuwa na Mkutano wa viongozi wa UWAKA wa Jumuiya zote leo Dominika 22.02.2026 mara baada ya Misa ya kwanza. |
| 8. | UCHAGUZI WA KAMATI TENDAJI | Uchaguzi wa Kamati Tendaji Parokia utafanyika Dominika ijayo 01.03.2026 mara baada ya Misa ya Kwanza. Tunaalikwa kuendelea kusali Novena ya kuomba ili kupata viongozi wa Parokia yetu. |
| 9. | GAZETI LA TUMAINI LETU | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuchukua Gazeti la Tumaini letu ofisini na kufanya malipo ya nakala 4 kati ya 5. |

## MASOMO YA DOMINIKA

## DOMINIKA YA 2 YA KWARESMA MWAKA A - TAREHE 01.03.2026

| | |
|---|---|
| SOMO I | Mwa 12: 1-4a |
| WIMBO WA KATIKATI | Zab 33:4-5, 18-20, 22 |
| SOMO II | 2Tim1:8b-10 |
| SHANGILIO | Mt 17:5 |
| INJILI | Mt 17:1-9 |